**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI ST. PAUL'S LIULI**
**S.L.P 07, LIULI-NYASA**

**Namba za Simu:**

| | |
|---|---|
| Mkuu wa Shule | **0621 37 75 95/0765 96 04 55** |
| Makamu Mkuu wa Shule | **0766 53 81 48** |
| Matron/Patron | **0765 47 63 33** |


**Tarehe 15/04/2024**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .________________________________
S.L.P _______________________________________________________

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ST. PAUL'S LIULI HALMASHAURI YA NYASA MKOA RUVUMA MWAKA 2024/2025.**

1. **Utangulizi**

   Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ..................................

   Shule ya Sekondari **ST. PAUL'S LIULI** ipo Mkoa wa Ruvuma, katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa. Ukiwa Songea, utapanda magari yanayoenda moja kwa moja **LIULI** kupitia Mbinga na Mbamba-bay. Tumia mabasi ya Kampuni ya Kisumapai Express au Kangaulaya. Umbali kutoka Songea Mjini hadi Liuli ni Kilometa 192. Nauli kutoka Songea ni Tshs 18,000. Shule imejengwa karibu na ufukwe wa Ziwa Nyasa.

   Aidha Usafiri wa basi kutoka Dar es salaam Kuja Mbamba bay ni Jumamosi kwa basi la Serous. Mabasi ya ***Superfeo*** na ***Serous*** hutoa huduma kila siku kutoka Dar es salaam kuja Songea na Mbinga pia kuna Usafiri wa meli kutoka Kyela ambao hutegemea hali ya ziwa kwa kipindi hicho. Kutoka Dodoma tumia usafiri wa basi la ***Superfeo***.

   Mwanafunzi atatakiwa kuripoti shule kuanzia tarehe **Itakayo tangazwa na Serikali.**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**

   **2.1. Sare za shule**

   **(i)** Mwanafunzi anatakiwa awe na Suruali mbili za bluu iliyoiva (dark blue), zenye marinda madogo mawili upande wa mbele na mfuko moja nyuma, pana na zinazofunika viatu, ziwe na pindo la chini (turn-up)

   **(ii)** Shati mbili nyeupe mikono mirefu, vishikizo vya kawaida (siyo chuma)

(iii) Sare za michezo ni bukta bluu (2), fulana bluu (2), track suit bluu (2) zenye michirizi myeupe, na raba nyeupe.

(iv) Viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili, visivyochongoka wala kuinuka kwa mbele na vyenye visigino vilivyoinuka kidogo.

(v) Soksi nyeupe (fupi) jozi mbili, sizizo na mapambo yoyote.

(vi) Mkanda wa ngozi mweusi wa suruali wenye "buckle" ndogo

(vii) Ndala au sandals haziruhusiwi kuvaliwa na sare.

(viii) Aje na nguo za kazi ambazo ni suruali mbili (2) za khaki zenye marinda madogo mawili upande wa mbele na mfuko mmoja nyuma, pana na zinazofunika viatu, ziwe na pindo la chini (turn-up)

(ix) Tai mbili fupi za bluu iliyoiva (rangi sawa na ya suruali)

(x) T - SHIRT ya rangi ya dark Bluu (2) (ambazo zitapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/= kwa **atakayetaka**).

(xi) Aje na sweta rangi ya bluu iliyoiva (dark blue) yenye shingo ya herufi V.

(xii) Vesti nyeupe mbili au zaidi.

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

(i) Madaftari 15 quire 3 au 4

(ii) Ream (A4) ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

(iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa);

(iv) Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

(v) Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma mathematics, chemistry na Geography;

(vi) Godoro futi 2 ½ x6x4. (yanapatikana katika duka la shule kwa shilingi 40,000/= kwa **atakayetaka**)

(vii) Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya bluu au nyeupe.

(viii) Nguo za ndani za kutosha

(ix) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

(x) Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

(xi) Kwanja 1, jembe 1, mfagio 1 wa ndani (soft bloom)

(xii) Koti la maabara 1(Lab. coat) rangi nyeupe kwa wanaosoma masomo ya sayansi.

(xiii) Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni

**2.3. Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango yote ilipwe benki kwenye Akaunti ya shule ***NMB 61701200083 ST. PAUL'S LIULI SECONDARY SCHOOL***. Shule **HAITAPOKEA FEDHA TASLIMU**.

Kabidhi risiti ya benki kwa Mhasibu ili upewe risiti ya shule pindi utakapofika shuleni.

***MUHIMU***

***Kwa asiye na kadi ya Bima ya afya aje na Tsh. 50,400/= tu taslimu siku anapowasili ili ikatiwe kadi ya Bima ya afya kwa mwaka mmoja. Gharama za matibabu ya mtoto ni za mzazi au mlezi mwenyewe.***

## 3. Sharia na Kanuni muhimu za shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1. Sheria na Kanuni za shule

- **(i)** Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- **(ii)** Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- **(iii)** Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
- **(iv)** Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- **(v)** Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- **(vi)** Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- **(vii)** Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- **(viii)** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- **(ix)** Kutunza mali za shule;
- **(x)** Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
- **(xi)** Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**ZINGATIA HAYA:**

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:-**

- **(i)** Wizi;
- **(ii)** Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
- **(iii)** Kugoma na kuhamasisha mgomo;
- **(iv)** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
- **(v)** Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
- **(vi)** Kufuga ndevu;
- **(vii)** Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
- **(viii)** Uvutaji wa sigara;
- **(ix)** Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa;
- **(x)** Kusababisha mimba;
- **(xi)** Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- **(xii)** Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
- **(xiii)** Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
- **(xiv)** Kudharau Bendera ya Taifa;
- **(xv)** Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
- **(xvi)** Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

**4.1. FOMU YA KUKUBALI AU KUKATAA KUJIUNGA NA SHULE HII**

**4.1.1** Mwanafunzi

- **(i)** Majina kamili (Matatu): ______________________________
- **(ii)** Shule ya O-level aliyosoma: __________________________
- **(iii)** Namba ya Mtihani (CSEE): ___________________________
- **(iv)** Tarehe ya kuzaliwa: _________________________________
- **(v)** Nakubali/Sikubali nafasi niliyopewa (kata lisilohusika)
- **(vi)** Nakili/naahidi kutokumiliki au kutumia simu shuleni, kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai.

  Saini ya mwanafunzi: ________________________________

**4.1.2 MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

- **(a)** Nakubali mwanangu apate elimu yake hapo shuleni
- **(b)** Na kwamba afuate sheria na maelekezo yote, vinginevyo aadhibiwe
- **(c)** Na kwamba mwanangu alelewe katika dini ya _______________
- **(d)** Na kwamba siafiki yeye kumiliki au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- **(e)** Na kwamba nitampa mahitaji yote yaliyoainishwa

**4.1.3** AFISA MTENDAJI WA KATA/KIJIJI/MTAA

Jina: ______________________ Kijiji/Kata/Mtaa ___________________

Wilaya _____________________ Mkoa: ___________________________

Nathibitisha kuwa mwanafunzi _____________________ ni wa kijiji/mtaa huu na ni raia wa TANZANIA

Saini na Muhuri ____________________________ Tarehe: ______________

**4.2 TAARIFA KAMILI ZA MWANAFUNZI**

**4.2.1** Jina Kamili: _______________________________________________________

**4.2.2** Tarehe ya kuzaliwa: _______ Dini: ___________ Dhehebu: _____________

**4.2.3** Mahali ulipozaliwa: _______________________________________________

**4.2.4** Shule ya msingi uliyosoma:____________ Mwaka uliomaliza: ___________

**4.2.5** Shule ya sekondari uliyosoma: ___________ Mwaka uliomaliza: _________

**4.2.6** Kidato unachokuja kuingia hapa: ____________________________________

**4.2.7** Jina la baba/mlezi: ______________________ Uhusiano: ________________ Kazi ya baba/mlezi: _________________ Dini: ________________ Namba ya Simu: ________________ Email: _________________________________ Anuani: ________________________________ Kijiji/mtaa/kitongoji/namba ya nyumba:___________________________ Kata:_______________________ Tarafa: ____________________ Wilaya: ___________________________ Mkoa: _____________________

**4.2.8** Jina la mama/mlezi: ______________________ Uhusiano: ________________ Kazi ya mama/mlezi: _________________ Dini: ________________ Namba ya Simu: ________________ Email: _________________________________ Anuani: ________________________________ Kijiji/mtaa/kitongoji/namba ya nyumba:___________________________ Kata:_______________________ Tarafa: ____________________ Wilaya: ___________________________ Mkoa: _____________________

**4.2.9** Kazi yeyote ya uongozi uliyowahi kuifanya
Madaraka/uongozi: ____________ Mahali/shule: ____________ Mwaka: ______

**4.2.10** Ndugu wa karibu wa mwanafunzi kama Baba, Mama, Kaka, Dada, Mjomba, Shangazi n.k aliyeko karibu na shule:

**(i)** **Jina la ndugu:** _____________ **Uhusiano:** _________ **Anapoishi:** _______ **Simu:** _______
**(ii)** **Jina la ndugu:** _____________ **Uhusiano:** _________ **Anapoishi:** _______ **Simu:** _______
**(iii)** **Jina la ndugu:** _____________ **Uhusiano:** _________ **Anapoishi:** _______ **Simu:** _______
**(iv)** **Jina la ndugu:** _____________ **Uhusiano:** _________ **Anapoishi:** _______ **Simu:** _______

Nathibitisha kwamba, habari zilizotolewa hapo juu ni sahihi, naahidi kuwa na tabia njema, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe________________ Sahihi ya mwanafunzi: _______________________

## SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(To be filled by the government medical officer)

Name of the student: ____________________________________________ Date: _____________

I shall be very grateful if you kindly examine the above named student and give us a report regarding her fitness to undertake studies well in our school.

### A. PRELIMINARY INFORMATION: MEDICAL INFORMATION

| S/N | DISEASE | YES | NO | S/N | DISEASE | YES | NO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **1.** | Tuberculosis | | | **9.** | Operation | | |
| **2.** | Asthma | | | **10.** | Eye disorder | | |
| **3.** | Pneumonia | | | **11.** | Diabetes | | |
| **4.** | Heart trouble | | | **12.** | Nervous breakdown | | |
| **5.** | Recurrent indigestion | | | **13.** | Ear/Nose/Throat trouble | | |
| **6.** | Kidney trouble | | | **14.** | Skin disorder/disease | | |
| **7.** | Anemia | | | **15.** | V.D | | |
| **8.** | Jaundice | | | **16.** | Disabled | | |

**VITAL STATUS**

Age:__________ Height: _________ Weight: _______ Blood group: _______________________

Blood pressure: _____________ Pulse rate ______ systolic:___________ Diastolic:___________

MEDICAL EXAMINATION

| | REMARKS/TREATMENT |
|---|---|
| EAR | RT LT |
| VISION | RT EYE LT |
| THROAT | |
| CHEST EXAMINATION | |
| ABDOMINAL EXAMINATION | LIVER SPLEEN |
| OTHER COMMENTS | |
| M.S SYSTEM | UPPER LIMBS |
| | LOWER LIMBS |
| | SKIN |
| ANY OTHER FINDINGS | |

LABORATORY EXAMINATION/INVESTIGATION

**1.** STOOL: OVA: ______________________________ Leucocytes: ______________________

**2.** URINALYSIS: Protein________________________ Glucose: _________________________

Sediment: OVA:__________________________________ Leucocytes: ______________________

**3.** Hb: ________________________________________

**4.** Bs: ________________________________________

**5.** VDRL: ____________________________________

**6.** WBC Total: _________________________________

Differential

N_________________________ L ________________________

M ________________________ E ________________________

B __________ ______________

**7.** X-ray chest (if any):

______________________________________________________________________

**8.** ANY OTHER INVESTIGATION

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**MEDICAL CERTIFICATION**

I have examined the above named student considered that he or she is physically fit/unfit for most activities taken at the school as my findings indicated above.

Date: ________________ Station: ______________________________________________________

Doctor's name: ____________________________________________ Signature: __________________

Thank you in advance

'THE HEADMASTER'
ST. PAUL'S LIULI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 07 LIULI NYASA

……………………………….

PAUL DAVID MWANDA
THE HEADMASTER

Telephone numbers:

**(i)** **0765960455**

**(ii)** **0621377595**

**ORODHA YA VITABU**

***01. History***

- *Major Issues in Africa* : *ICD*
- *Major events in African History* : *Mwaijage*
- *The political economy Imperialism* : *Nabudere*
- *Africa Since 1800. 4th edition* : *Roland Oliver Atmore*
- *The making of Modern Africa. Vol.1*
- *How Europe under developed Africa* : *Walter Rodney*
- *The 20th century* : *Duff, M.N*
- *Europe from 1815* : *Pea Cock*

***02. Geography***

- *Certificates of Geography (Oxford)* : *Marry Mugo ,Robert Karugga, Paul Kibuuka*
- *General Geography in Diagrams* : *R.B. Bunnet*
- *Regional Geography* : *Nyangwine/Msabila*
- *Photograph interpretation and Elementary* : *S.E. Dura*
- *Surveying for Secondary level, New edition*
- *Certificate of human and Economic Geography* : *Morgans and Leong Chang*
- *Principles in Physical Geography* : *Monk House*
- *Geography-An Intergrate Approach* : *David Waugh (2009)*
- *Practical Geography* : *Pritchard*

***03. English Language***

***Paper 1***

- *A Complete English Course for Form Six* : *Michael Kadeghe*
- *English for Form V and VI* : *Michael Kadeghe*
- *Teaching English as a Foreign Language* : *G. Broughton*
- *Longman Grammar* : *L.G Alexander*
- *Advanced Learner's Dictionary* : *Oxford University Press*

***Paper 2***

***Novels***

- *The Beautyful One's are Not Yet Born* : *A.K. Amah*
- *The Grain of Wheat* : *Ngugi wa Thiong'o*
- *A Man of the People* : *Chinua Achebe*
- *Vanishing Shadow* : *N. Kayombo*
- *His Excellency the Head of State* : *Danny B Safo*

***Plays***

- *Betrayal in the City* : *Francis Imbuga*
- *An Enemy of the People* : *Henrik Ibsen*
- *Lwanda Magere* : *Okoiti Omtatah*
- *I will Marry when I want* : *Ngugi wa Thiong'o & Mirii*

***Poetry***

- *Selected poems* : *Institute of Education*
- *Growing up with poetry* :
- *Summons* : *Richard Mabala*

***04. KISWAHILI***

***Tamthiliya***

- *Morani* :
- *Kivuli kinaishi* :
- *Kwenye Ukingo waThim* :
- *Nguzo Mama* :

***Riwaya***

- *Usiku utakapokwisha* :
- *Vuta N'kuvute* :
- *Mfadhili* :
- *Kufikirika* :

***Mashairi***

- *Fungate ya Uhuru* :
- *Mapenzi Bora* :
- *ChunguTamu* :
- *Kimbunga* :

***VITABU VINGINE VINAVYOHITAJIKA***

***A. Geography***

- *Map Reading* : *Dura S.E*
- *Map Reading for East Africa* : *D.N. Mc Master*
- *First lessons in Reading* : *Pritchard J.M*
- *Earth Science* : *Emilian .C. Knight, L.B. and Hand Weker, M.(1989).*

***B. History***

- *Modern World History* : *Chance .M. and Writte, J.(1950*
- *Topics in West African History* : *Boahen, A. (1997*
- *World Civilization* : *Adm, G.(1970).*
- *The Evolving World* : *Kiruti, F. (2000)-*
- *Modern World History* : *Nigel Kelly and Grey Lacey (2001*
- *A History of Africa* : *Assa Okoth-*

***C. English Language***

- *English for form V and VI* : *Oxford*
- *Advance English Revised edition* : *Ashel*
- *The Wonderful Surgeon and other poem* : *Charles Mloka*
- *Advanced level Literature* : *Nyambari Nyangwine*

***VITABU VYA SAYANSI***

***A. Chemistry***

- *Advanced level Physical Chemistry with General Chemistry* : *Ape Network*
- *Chemistry for A' level and 1st year undergraduate students*

*Inorganic Chemistry Part A& B* : *(By J.S MARO – AND MIKESEWALLA) Mzumbe Book Project.*

- *Conceptual Chemistry, Class XI & XII* : *By S. CHAND*
- *A' Level Chemistry, 4th Edition* : *E.N RAMSDEN*
- *Organic Chemistry Part A & B* : *MZUMBE BOOK PROJECT*

***D. Biology***

*Understanding Biology 4st Ed,* : *Glenn and Susan Toole. Stanley Thomes 1999.*
*Biological Science 3rd Ed.* : *D Tylor. NPO Green and Stout*
*Guidance to dissection* : *H.G.Q ROWETT H.*
*Advanced Level Biology, text book form V and VI* : *Ernest Kira 2009*

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

**Namba za Simu:**

| | |
|---|---|
| Mkuu wa Shule | **0621 37 75 95/0765 96 04 55** |
| Makamu Mkuu wa Shule | **0766 53 81 48** |
| Matron/Patron | **0765 47 63 33** |




……………………………
PAUL DAVID MWANDA
MKUU WA SHULE